THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

KISWAHILI FOR LEARNERS WITH PHYSICAL DISABILITIES

# Monitoring Learner Achievement at Primary School Level in Kenya

## Darasa la 8

© KNEC 2020

GEUZA UKURASA

**JINA** ______________________________________________________________

**NAMBA YA USAJILI** ________________________________________

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO.**

1. Kijitabu hiki kina maswali **50**.
2. Hakikisha ya kwamba umeandika jina lako na namba yako ya usajili.
3. Umepewa muda wa saa 1 dakika 40 kujibu maswali yote.
3. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu **manne**. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahii. chagua jibu hilo.
4. Chora kiduara au pigia mstari herufi ambayo ndilo jibu lako.

   **21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
   A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo
   (B.) njuga, tari, kinubi, fidla
   C. harimuni, marimba, msondo, maleba
   D. siwa, zeze, upatu, nembo.
   Jibu sahihi ni B. Jibu hili ndilo lililochorewa kiduara.
5. Pigia mstari au chorea kiduara kwenye jibu **moja** tu.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**KIGEZO** (50 marks)

| **SWALI** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** | **9** | **10** | **11** | **12** | **13** | **14** | **15** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **ALAMA** | | | | | | | | | | | | | | | |

| **SWALI** | **16** | **17** | **18** | **19** | **20** | **21** | **22** | **23** | **24** | **25** | **26** | **27** | **28** | **29** | **30** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **ALAMA** | | | | | | | | | | | | | | | |

| **SWALI** | **27** | **28** | **29** | **30** | **31** | **32** | **33** | **34** | **35** | **36** | 41 | 42 | 43 | 44 | 45 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **ALAMA** | | | | | | | | | | | | | | | |

| **SWALI** | **37** | **38** | **39** | **40** | **41** | **42** | **43** | **44** | **45** | **46** | **47** | **48** | **49** | **50** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 50 |
| **ALAMA** | | | | | | | | | | | | | | | |

**© KNEC 2020**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* ***1*** *mpaka* ***15****. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo* ***zaidi*** *kati ya yale uliyopewa.*

Ni jambo la busara kuishi kulingana na uwezo **__1__** **__2__**. Kila mja huwa **__3__** _ kwa njia anuwai. Si vizuri **__4__** na wenzako kwani **__5__.** Mwalimu wetu alitushauri **__6__** kwa kila jambo. **__7__** Utasumbuka usiposhirikiana na wenzako. Kumbuka tunapaswa kufaana kwa shughuli **__8__** tunafanya kila siku. Tukifanya hivyo, tutaishi maisha bora.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. wetu | B. wao | C. wako | D. wenu |
| **2.** | A. yenyewe | B. mwenyewe | C. lenyewe | D. kwenyewe |
| **3.** | A. alijaliwa | B. angejaliwa | C. atajaliwa | D. amejaliwa |
| **4.** | A. kushindia | B. kushindiana | C. kushindiwa | D. kushindana |
| **5** | A. mtu hujikuna ajipatapo | | B. mcheza kwao hutuzwa | |
| | C. mtegemea cha nduguye hufa maskini | | D. mtaka cha mvunguni sharti ainame | |
| **6.** | A. tutie moyo | B. tutie fora | C. tutie shime | D. tutie mkazo |
| **7.** | A. Maskini! | B. Kefule! | C. Hewala! | D. Lahaula! |
| **8.** | A. ambao | B. ambalo | C. ambapo | D. ambazo |

Shule **__9__** mwanafunzi milango ya ufanisi **__10__** maisha ya usoni. Kila taaluma **__11__** ipasavyo huko shuleni. **__12__** vipaji vingi hukuzwa miongoni mwa wanafunzi. Kuna mambo mengi ambayo mwanafunzi anahitaji kuwa nayo **__13__** bidii, nidhamu na stahamala. Kufaulu maishani **__14__** elimu bora inayompa mwanafunzi **__15__** za maisha.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. humfungulia | B. hukufungulia | C. hutufungulia | D. hunifungulia |
| **10.** | A. kwenye | B. licha ya | C. baada ya | D. katika |
| **11.** | A. zinapaliliwa | B. inapaliliwa | C. unapaliliwa | D. mnapaliliwa |
| **12.** | A. Angalau | B. Halafu | C. Maadamu | D. Vilevile |
| **13.** | A. **;** | B. **:** | C. **,** | D. **.** |
| **14.** | A. kunategemeka | B. kunategemezwa | C. kunategemea | D. kunategemewa |
| **15.** | A. stadi | B. kauli | C. shabaha | D. hatua |

*Kutoka nambari **16** hadi **30**, chagua jibu sahihi.*

**16**. Ni neno lipi lenye sauti mwambatano?
A. Mvua
B. Mwalimu
C. Daftari
D. Fahamu

**17**. Onyesha kiwakilishi katika sentensi ifuatayo.
Kupi kulikopandwa miti mingi?
A. kuliko
B. miti
C. mingi
D. kupi

**18**. Wingi wa sentensi ifuatayo ni:
Utakaponufaika kutokana na kazi za vikundi utavithamini zaidi.
A. Watakaponufaika kutokana na kazi za vikundi utavithamini zaidi.
B. Watakaponufaika kutokana na kazi ya vikundi mtavithamini zaidi.
C. Mtakaponufaika kutokana na kazi za vikundi mtavithamini zaidi.
D. Mtakaponufaika kutokana na kazi ya vikundi utavithamini zaidi.

**19**. Chagua kukanusha kwa:
Maarifa akifika tutashauriana.
A. Maarifa asipofika hatutashauriana.
B. Maarifa asipofika tutashauriana.
C. Maarifa hatafika lakini tutashauriana.
D. Maarifa atafika ila hatutashauriana.

**20**. Ni sentensi ipi yenye ***'ka'*** inayoonyesha mfuatano wa vitendo?
A. Kadzo alifika nyumbani akachukua kitabu akaanza kusoma.
B. Nenda ukaoshe hanchifu ya mtoto.
C. Atakapowasili nitakujuza.
D. Tulicheza uwanjani kwa muda tukanyoosha viungo vyetu.

**21**. Chagua neno lifaalo kujaza pengo.
Milka atakuonyesha ____ viazi hivyo.
A. alipopika
B. aliopika
C. alivyopika
D. aliyopika

**22**. Chagua sentensi yenye ***'na'*** ya kumiliki.
A. Tunaunda kikundi chetu.
B. Matunda yalinunuliwa na mama.
C. Nina vitabu vyote vya kusoma.
D. Mimi na yeye tutasaidiana.

**23**. Neno **paa** lina maana hizi zote isipokuwa:
A. ruka angani
B. chukua makaa ya moto kutoka kwenye jiko
C. mnyama wa porini anayefanana na mbuzi
D. sehemu ya mbele ya uso

**24**. Kivumishi kilichopigiwa mstari kimeundwa kutokana na aina gani ya neno?
Mwalimu <u>mshindi</u> ametuzwa.
A. Kielezi
B. Kiwakilishi
C. Kihusishi
D. Kitenzi

**25**. Tabia za Jumba na Jomba zimetofautiana kama
A. usiku na mchana
B. maji na mafuta
C. ardhi na mbingu
D. kuku na mwewe

**26**. Mzinga ni kwa nyuki kama vile ____ni kwa mchwa.
A. kiota
B. kitala
C. kibanda
D. kichuguu

**27**. Methali zifuatazo zinalingana kimaana, isipokuwa?
A. Kwendako mema hurudi mema.
B. Kumpa mwenzio si kutupa.
C. Ndugu mui heri kuwa naye.
D. Jaza ya hisani ni hisani.

**28**. Neno **karibu** katika sentensi ifuatayo lina maana gani?
Tulitumia karibu shilingi elfu tatu safarini.
A. pengine
B. takriban
C. nusura
D. kufikia

**29**. Chagua sentensi iliyounganisha sentensi zifuatazo ifaavyo.
Utaepuka magonjwa.
Dumisha usafi.
A. Utaepuka magonjwa ilimradi udumishe usafi.
B. Utaepuka magonjwa madhali udumishe usafi.
C. Utaepuka magonjwa mintarafu udumishe usafi.
D. Utaepuka magonjwa ilhali udumishe usafi.

**30**. Chagua sentensi iliyo katika usemi wa taarifa.
"Tutaenda kucheza baada ya masomo," wanafunzi walisema.
A. Wanafunzi walisema kwamba mtaenda kucheza baada ya masomo.
B. Wanafunzi walisema kwamba wangeenda kucheza baada ya masomo.
C. Wanafunzi walisema kwamba wataenda kucheza baada ya masomo.
D. Wanafunzi walisema kwamba tungeenda kucheza baada ya masomo.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **31** hadi **40**.*

Kila mwanadamu ameumbwa akiwa na uwezo wake maalum. Mungu alifanya hivyo makusudi kabisa. Hebu fikiria ulimwengu wenye watu ambao kila mmoja anajitosheleza! Yaani, kila mtu anaweza kujifanyia kila kitu apendavyo. Ulimwengu usingehitaji watu wanaosomea kazi mbalimbali wala watu wasingetegemeana. Upendo na huruma vingekuwa havipo duniani.

Mungu aliwaumba watu na vipawa vyao mbalimbali. Hata wanaofikiriwa kuwa hawana vipawa, ukiwachunguza vizuri utaona kuwa wana upekee fulani katika jambo **wanalolimudu** vizuri. Wakati mwingine, sio lazima jambo hilo liwe kubwa sana kiasi cha watu kulizungumzia. Kuna watu wasiokuwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi lakini waliobarikiwa kwa uwezo wa kuzungumza vizuri au uwezo wa kuwashauri wengine wenye mahitaji mbalimbali. Hili linatukumbusha kuwa hata vipawa tunavyofikiri kuwa si vikubwa vina thamani kubwa ajabu.

Ingawa kila mtu ana kipawa chake, kuna watu wengi wasioweza kutambua vipawa vyao. Sababu moja inayowafanya washindwe kutambua vipawa hivyo ni kule kutokuwa na mtu wa kuwaongoza na kuwahimiza kuandama safari ya vipawa vyao. Sababu nyingine ni kwamba, watu wengine hawaviamini wala kuvithamini vipawa vyao. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa na kipawa cha kucheza kandanda lakini akawa anataka kuwa daktari hata kama huo udaktari haumo katika damu yake. Mtu anapopuuza kipawa chake na kukifuata kingine tofauti, huwa hana hamu na raha ya kufanya kazi ambayo hatimaye atakuwa amechagua kuifanya.

Wakati mwingine watu hupotoshwa kuviacha vipawa vyao. Jamaa na marafiki huweza kumshawishi mtu kukiacha kipawa chake na badala yake kukifuata kile cha wale wanaomshauri. Mara nyingi wanaomshawishi mtu kuacha kipawa chake huwa hata hawajauelewa uwezo wa wanayemshauri. Hatimaye mkondo mpya anaoufuata unamnyima nafasi ya kukuza kipawa chake alichopewa na Mungu. Japo watu wengine hufanikiwa kwa kuelekezwa kufuata njia ambayo haikuwahusu, wengine hushindwa kufanikiwa vizuri maishani. Hata katika hao wanaofanikiwa, huwa kuna asilimia kubwa inayojilazimisha kuifanya kazi ambayo haihusiani na talanta yao moja kwa moja. Kazi hiyo waifanyayo huwakosesha raha.

Ni vizuri kutambua kwamba, kuwa na kipawa tu hakutoshi. Kipawa cha mtoto ni mche unaohitaji maji, mwanga na mazingira mazuri yasiyo na magugu ili uweze kuimarika na kustawi, lau sivyo utanyauka na kukauka. Mwenye kipawa anafaa kukilea kwa kukifanyia mazoezi ili kukiboresha. Anafaa kuwa na nidhamu ya kukiendeleza hadi kitakapokomaa. Anahitaji kufuata ushauri na mwongozo wa watu wengine ambao wamekitumia vizuri kipawa sawa na chake. Kwa kufanya hivi kipawa kitakuwa kimepaliliwa vizuri na matunda yake yatakuwa wazi na tayari kuvunwa kwa manufaa ya mwenye kipawa na jamii kwa jumla.

Tunafaa kutambua kuwa vipawa ni vingi jinsi walivyo watu. Vilevile hata watu wenye kipawa kile kimoja wana uwezo tofauti. Kama wasemavyo wahenga, **akili ni nywele na kila mtu ana zake**. Hii ndio maana tunakumbushwa daima dawamu kuwa hata vidole havilingani. Kila kimoja kina umbo na urefu wake unaokifanya kutegemewa na vingine.

**31**. Chagua jibu sahihi kulingana na aya ya **kwanza.**
- A. Bila kuwa na elimu wanadamu hawawezi kusaidiana.
- B. Kila binadamu ana mambo maalum anayopenda.
- C. Watu wanaojifanyia kila kitu huwashangaza wanajamii.
- D. Hali ya kutegemeana husaidia kujenga maadili.

**32**. Kwa mujibu wa aya ya **pili:**
- A. Watu wengi hudhani kuwa wengine hawana vipawa.
- B. Kuna vipawa vya thamani kuliko vingine.
- C. Wakati mwingine watu wenye vipawa hawagunduliwi.
- D. Wasiokuwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi wamebarikiwa.

**33**. Kifungu kinaonyesha kuwa watu wengi hawawezi kutambua vipawa vyao kwa sababu:
- A. Huwa hawafurahishwi na vipawa vyao kama wenzao.
- B. Hukosa mwongozo unaofaa wa kukuza vipawa vyao.
- C. Huwaza kuwa kutambua vipawa kunachukua muda mrefu.
- D. Hufikiri kuwa kipawa cha udaktari ndicho bora maishani.

**34**. Ni kauli ipi **sahihi** kulingana na kifungu?
- A. Wasiojua umuhimu wa kazi huwazuia wengine kushughulikia kazi zao.
- B. Kubadilisha kazi huifanya isiwe ya kuvutia kwa wale wanaoifanya.
- C. Jamaa na marafiki huweza kumnyima mtu fursa ya kukuza kipawa chake.
- D. Wanaotoa ushauri kuhusu thamani ya vipawa huwa wanawajua wenye vipawa hivyo.

**35**. Kifungu kimebainisha kuwa:
- A. Watu hufanya vizuri kuwashauri wengine kuacha vipawa vyao.
- B. Ushawishi wa marafiki huwa mkubwa zaidi kuliko wa wenye talanta.
- C. Baadhi ya wanaoshauriwa kufuata talanta tofauti na zao hufaulu maishani.
- D. Ukuzaji wa vipawa hutofautiana kulingana na imani ya mtu kwa Mungu.

**36**. Mwandishi anapendekeza njia za kukuza vipawa. Chagua pendekezo ***lisilo sahihi*** kulingana na kifungu. Mwenye kipawa
- A. anahitaji kukifanyia mazoezi ili kukiboresha.
- B. anahitaji kuhakikisha amekiimarisha hadi kitakapokomaa.
- C. anafaa kufuata mfano wa wengine wenye vipawa sawa na chake.
- D. anafaa kuwategemea walio karibu naye ili kukijenga kipawa chake.

**37**. Chagua matatizo ambayo yanaweza kumkabili mtu anayetaka kukuza kipawa chake kwa mujibu wa kifungu.
- A. kupuuza uwezo wao, kufuata wafanyayo wengine
- B. kutamani makuu, kukosa uvumilivu
- C. kuwa na woga, kukosa wa kumwelimisha
- D. kuwa na washauri, kudharau michezo

**38**. Kauli zifuatazo zimetumiwa katika kifungu. Ipi iliyotumia sitiari?
- A. Kipawa cha mtoto ni mche unaohitaji maji, mwanga na mazingira mazuri.
- B. Hebu fikiria ulimwengu wenye watu ambao kila mmoja anajitosheleza!
- C. Hii ndio maana tunakumbushwa daima dawamu kuwa hata vidole havilingani.
- D. Hatimaye mkondo mpya anaoufuata unamnyima nafasi ya kukuza kipawa chake.

**39**. Katika kifungu, maana ya methali, '**Akili ni nywele, kila mtu ana zake**' ni:
- A. Viwango vya uwezo wa watu vinatofautiana.
- B. Watu wenye hamu ya kushirikiana hutofautiana.
- C. Mitazamo ya watu kuhusu vipawa hutofautiana.
- D. Watu wanaothamini vipawa wanatofautiana.

**40.** Chagua maana ya neno ***'wanalolimudu'*** kama lilivyotumiwa katika kifungu.
- A. wanalolipenda
- B. wanaloweza kulifanya
- C. wanaloliamini
- D. wanalofurahia kulitenda

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Habari zilikuwa zimeenea kila mahali kuhusu Pablo; kijana mdogo aliyefika kijijini kwetu kutoka mjini. Pablo alikuwa na sifa nyingi. Hali hii iliwafanya watu kijijini kuchukulia kuwa Pablo alikuwa na uwezo usio wa kawaida. Wengine waliona kuwa alikuwa mtoto wa ajabu huku wengine wakichukulia kuwa Pablo mwenyewe alikuwa muujiza. Lakini amini usiamini, kwangu mimi Pablo alikuwa binamu yangu. Nilijua kwao. Mama yake ni mdogo wa baba yangu, wote wakiwa watoto wa Mzee Mamboshwari na Bi.Sasatulia.

Pablo alipofika kutoka mjini, alikuja na jina la ajabu, yaani Pablo. Watu wengi kjijini walishindwa kulitamka jina lake. Kwa hivyo walimwita Bopiro. Baadhi walimwita Boflo. Pablo hakuitika majina hayo. Alinyamaza tu na kuwatazama watu. Alipoulizwa kwa nini hapendi kuitika alijibu, "Mimi ni Pablo." Hapo basi tulibaki tunavunjika mbavu kwa vicheko. Wengi hawakuelewa tofauti ya Pablo na Bopiro au Boflo. Baadhi ya walioelewa walijaribu kulitamka jina lake Pablo ilivyofaa na ulimi ulipoteleza na kutamka visivyo, walijitahidi kujisahihisha haraka kwa kulitamka tena vizuri – Pablo.

Huyu binamu yangu alipofika kijijini alikuwa hajui maneno mengi ya lugha yetu ya kiasili. Kwa hivyo, watu waliposema naye, Pablo alibaki ameduwaa tu. Mara nyingi alitabasamu na kutazama chini. Kuna watu waliouliza, "Kwa nini wazazi wake Pablo hawajamfundisha lugha ya kiasili?" Sisi hatukuwa na jibu. Pablo hata hakuwa na habari tena kwa sababu alikuwa mbioni kuwafukuza vipepeo waliojipamba kwa rangi za kuvutia. Ingawa Pablo alipenda sana kufukuzana na vipepeo, mara kwa mara alisahau kuwafuata alipoona maua ya miti mbalimbali. Aliyachuma maua hayo ya rangi mbalimbali na kuyatia mfukoni mwake. Mara nyingi nilikuwa karibu naye asije akalishika ua lenye nyuki au kushika mimea inayowasha ama yenye ncha kali.

Pablo alikuwa anachekesha kweli. Kuchekesha kwake kulitokana na mambo mengi aliyofanya. Kuna siku alimwendea babu akamwambia kuwa angependa kwenda kulima. Wakati huo ulikuwa mwendo wa saa kumi na mbili jioni. Jua lilikuwa limeanza kutua na ng'ombe walikuwa wanarudi kutoka malishoni. Mvua iliyokuwa imenyesha ilikuwa imeufanya udongo kulowa na kufanya donge zito. Babu alicheka kidogo kisha akaniambia, "Mlajasho, mpe bwana mdogo jembe akalime." Nilitii na kumpa Pablo jembe alilolibeba huku limemlemea. Aliliinua likaenda juu chini mara kadha nalo likawa limeshika tope zito. Alishindwa kuliinua. Nilifika mara kwa mara kumwondolea dongo lililolisakama jembe. Baada ya muda alikuwa amechoka. Alibaki kuhema. Vidole vyake vya mkono viliuma. Nguo zake safi sasa zilikuwa chafu na kiatu chake kimoja kilikuwa kimemtoka. Kilikuwa kimejizika ndani ya udongo. Watoto waliokuwa pale nyumbani walicheka sana lakini Pablo alifululiza ndani na kumweleza babu kuwa alikuwa amekamilisha kazi yake na kwamba kesho yake angeenda kupanda mbegu. Sote tulicheka hadi tukatiririkwa na machozi.

Siku iliyofuata Pablo alikuwa amesahau alifaa kwenda kupanda mbegu shambani. Badala yake, alichukua mfuko wake wa vitabu na kuchomoa kitabu cha hadithi. Alituamrisha kukaa kimya. Sote tulitii. Babu aliyekuwa ameketi pembeni kabisa alikuwa anatikisa kichwa kama anayekubaliana naye. Pablo alianza kutusomea hadithi aliyoipenda sana kuhusu farasi mwenye bidii na sungura mjanja asiyependa kufanya kazi. Alipomaliza kila mmoja alibaki ameshangaa. Pablo alikuwa anajua kusoma kwa ufasaha mkubwa. Wale watoto waliokuwa wakimcheka Pablo alipokuwa akilima wote walinyamaza. Waliajabia uwezo wake Pablo. Hata mimi nilishangaa. Nilitambua kuwa ukiujua huu na ule huujui. Habari hizi za Pablo zilienea kote kijijini kama moto nyikani wakati wa kiangazi.

Japo uwezo wa Pablo kuwasomea wengine hadithi uliwafanya watu kijijini kushangaa, kuna jambo lingine lililowafanya watu kuamini kuwa alikuwa mtoto wa miujiza. Pablo alikuwa na uwezo wa kukumbuka hadithi nyingi alizosoma na zile alizotazama na kusikiliza mtandaoni. Aliwavutia watu wengi. Watoto wenzake walimpenda sana nao wazazi ambao walikuwa hawana mazoea ya kuwanunulia watoto wao vitabu vya kusoma nyumbani, walilazimika kuwanunulia. Kila mmoja alitaka mtoto wake awe kama Pablo. Kabla ya likizo kumalizika, wazazi wa kijiji chetu walikuwa wameungana kununua vitabu. Waliandaa ratiba ya watoto kukutana na kusomeana hadithi mara tatu kwa wiki.

**41**. Kulingana na aya ya **kwanza**:
A. Wanakijiji walikuwa wamepata habari za kushangaza kuhusu kufika kwa Pablo.
B. Msimulizi alikuwa na maoni tofauti na wanakijiji kumhusu Pablo.
C. Ukoo wa Pablo ulimfanya kuwa na uwezo wa kipekee.
D. Wazazi wa Pablo walikuwa wamemfunza mbinu nyingi za kufanya mambo.

**42**. Aya ya **pili** imebainisha kwamba:
A. Pablo na watu wengine wa mjini wana majina magumu kutamka.
B. Wenzake Pablo walikuwa hawajawahi kulisikia jina hilo.
C. Pablo aliwafanya baadhi ya watu wajitahidi kulitamka jina lake vizuri.
D. Watu walicheka kwa sababu Pablo alikataa kuitika jina lake lilipotamkwa vibaya.

**43**. Katika aya ya **tatu** Pablo:
A. Alikuwa hapendi kuzungumza.
B. Anayafurahia mazingira mapya.
C. Aliiona mimea mbalimbali kuwa ya ajabu.
D. Alikuwa haithamini sana lugha ya kiasili.

**44**. Msimulizi amewajibika kwani
A. hakulalamikia hali ya wazazi wa Pablo kutomfunza lugha ya kiasili.
B. alimlinda Pablo dhidi ya mimea iwashayo na wadudu wenye madhara.
C. alitambua hamu ya Pablo ya kucheza na vipepeo.
D. hakushangaa Pablo aliposhindwa kuinua jembe lenye tope.

**45**. Kulingana na hadithi, ni shughuli gani ambayo watu wa kijijini waliendeleza?
A. kufuga ng'ombe
B. kuvuna maua
C. kuuza asali
D. kupalilia miti

**46**. Wazo kuu linalojitokeza katika aya ya **tano** ni:
A. Kushindwa kutekeleza jambo fulani hakumaanishi huwezi lingine.
B. Kusoma kwa ufasaha ni bora kuliko kujishughulisha na kazi za kilimo.
C. Iwapo umesahau kufanya jambo ulilolipangia unaweza kufidia kwa kusoma.
D. Ukiona umechelewa kukamilisha kazi jua kwamba wengine wanajaribu kama wewe.

**47**. Ni ipi ambayo **si** sifa ya wazazi wa kijiji hiki kwa mujibu wa kifungu? Ni wenye
A. kuaminika
B. kujali masilahi
C. kushirikiana
D. kupenda hadithi

**48**. Chagua manufaa ya ziara ya Pablo kijijini kwa mujibu wa aya ya sita.
A. Iliwafanya wanakijiji waanze kupangia shughuli zao
B. Iliwasaidia watoto wa kijijini kuongeza idadi ya mikutano yao kwa wiki.
C. Iliwahamasisha vijana kuhusu faida za mtandao.
D. Iliwazindua wazazi kutambua umuhimu wa kuwajengea watoto wao stadi ya kusoma.

**49**. Chagua jibu lenye mpangilio ufaao wa matukio kulingana na jinsi yalivyotokea kwenye hadithi.
i. Pablo alifika kijijini kutoka mjini.
ii. Wazazi wa Pablo hawakumfunza lugha ya kiasili.
iii. Babu alitikisa kichwa kama mwenye kukubaliana na Pablo.
iv. Watoto walikutana kusomeana hadithi kutoka vitabuni.
v. Pablo alitaka kwenda kulima wakati wa jioni.

A. (i), (ii), (iv), (v), (iii)
B. (ii), (i), (v), (iii), (iv)
C. (i), (iii), (v), (iv), (ii)
D. (ii), (iv), (i), (iii), (v)

**50**. Kauli zifuatazo zimetumiwa kwenye hadithi. Ni ipi iliyotumia chuku?
A. Ulimi ulipoteleza na kutamka visivyo.
B. Tulibaki tunavunjika mbavu kwa vicheko.
C. Mlajasho, mpe bwana mdogo jembe akalime.
D. Zilienea kote kijijini kama moto nyikani wakati wa kiangazi.